



TAMKO LA WIZARA YA AFYA KUHUSU UGONJWA WA EBOLA

Ndugu Wananchi, Siku ya tarehe 20 Septemba 2022, Wizara ya Afya ilipokea taarifa iliyotolewa na Waziri wa Afya wa Uganda, kupitia vyombo mbalimbali vya habari juu ya mripuko wa ugonjwa wa Ebola katika Wilaya ya Mubende na Wilaya zingine tatu nchini humo. Mnamo tarehe 21 Septemba, 2022 wizara ilitoa tamko la kuhabarisha umma pamoja na kutoa tahadhari juu ya ugonjwa huu kwa wananchi ikiwemo hatua za kuchukua ili kujikinga. Hadi kufikia tarehe 29 Septemba, 2022, jumla ya **wagonjwa 54 walithibitika kuwa na ugonjwa huo na vifo 25 vilikuwa vimetolewa taarifa nchini Uganda.**

Ndugu wananchi, Tarehe 01 Oktoba, 2022, Wizara ya Afya imepokea taarifa kutoka Wizara ya mambo ya nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki ikithibitisha kifo cha mmoja wa wanafunzi ambaye alipata maambukizi ya Ebola (**Dkt. Mohamed Ali Hafidh**) aliyekuwa akisomea udaktari bingwa wa upasuaji (**Master of Medicine in general surgery**) nchini Uganda akitokea Tanzania (Zanzibar) kilichotokea wakati akipatiwa matibabu katika hospital ya Fort Portal Ishaka RRH.

Ndugu Wananchi, Kutokana na taarifa hizi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara ya Afya inatoa pole kwa wafiwa wote kwa kuondokewa na mtaalamu ambaye ni nguvu kazi ya taifa aliekwawa na mauti akiwa katika majukumu ya kikazi. Wizara ya Afya inaendelea kuwasiliana kwa karibu na serikali kupitia Wizara ya Afya Uganda ili kuona namna bora

ya kuhakikisha taratibu zote stahiki zinafuatwa pamoja na familia kuongozwa namna ya kushughulikia jambo hili huku tukiendelea kuhakikisha maambukizi hayaingii nchini.

Ndugu wananchi, Hadi sasa hapa nchini hakuna mgonjwa yoyote aliyehisiwa au kuthibitishwa kuwa na virusi vya Ebola. Tunatambua kuwa ugonjwa huu unaendelea kuripotiwa kwa kasi nchini Uganda na kutokana na muingiliano wa watu hususan wanafunzi wanaosoma vyuo mbali mbali nchini humo na wananchi wanaoingia nchini kwa shughuli za kibiashara na kijamii kunaiweka nchi yetu kuwa katika hatari kubwa ya maambukizi ya virusi vya Ebola.

Hivyo, hatuna budi kuchukua tahadhari ya hali ya juu ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu. Dalili kuu ni homa kali, mwili kuchoka, kuumwa viungo vya mwili, vidonda katika koo, kuharisha na kutokwa damu katika matundu ya mwili yaani puani, mdomoni, masikioni, machoni na njia ya haja kubwa na ndogo hali inayopelekea kifo ndani ya muda mfupi. Njia kuu za kujikinga na ugonjwa huu ni pamoja na Kuepuka kugusa au kuingiwa na mate, damu, mkojo, jasho, kinyesi, machozi na majimaji mengine yanayotoka mwilini mwa mgonjwa wa Ebola, Kuepuka kushughulikia maiti ya mtu aliyefariki; badala yake watoe taarifa kwa uongozi wa kituo cha huduma za Afya kwa ushauri na kuepuka kusafiri pasipokuwa na ulazima kwenye nchi zilizothibitika kuwa na ugonjwa huu.

Ndugu wananchi, Wizara ya Afya inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuzuia ugonjwa huu usiingie nchini zikiwemo;

- i. Kuandaa mpango mkakati wa kujiandaa na kupambana na mlipuko wa Ebola endapo utatokea nchini.

- ii. Kuendelea kuelimisha umma kupitia vyombo mbalimbali vya habari.
- iii. Kuhakikisha dawa, vifaa na vifaa tiba muhimu vinakuwepo katika vituo vya kutolea huduma za afya.
- iv. Kuimarisha uchunguzi wa wasafiri katika mipaka hasa kwenye maeneo makuu ya kuingia Zanzibar (Viwanja vya ndege na Bandari zote rasmi na zisizo rasmi)
- v. Kuimarisha ufuatiliaji wa tetesi za watu wenye viashiria vya ugonjwa kwenye jamii na vituo vya kutolea huduma za afya.
- vi. Kuhakikisha uwepo wa vituo vya kuwahudumia wagonjwa watakao thibitika.
- vii. Kuimarisha mfumo wa usafirishaji na upimaji wa sampuli katika maabara ya Taifa ya Afya.

Ndugu wananchi, Nahitimisha kwa kutoa rai kwa kila mwananchi ambaye anaingia nchini kutoka nchini Uganda au nchi nyengine yenye maambukizi ya Ebola kutoa taarifa ili kusaidia ufatiliaji wa ugonjwa huu kupitia vituo vya afya vilivyo karibu ili aweze kupewa muongozo sahihi na hatua za kufuata.

Kwa maswali au kutoa taarifa wasiliana na wataalamu wetu kupitia namba **190 au +255777952636/+255773208578**

Chukua Hatua Mapema, Ebola Inazuilika, Kinga ni Bora kuliko Tiba!



Nassor A. Mazrui (MBL)

Waziri wa Afya